**JINA: …………………………………. NAMBARI: ………….. KIDATO: ……….**

**KISWAHILI**
**KIDATO CHA KWANZA**
**MUHULA WA KWANZA**
**MUDA: SAA $1^{1/2}$**
**ALAMA 50**

## A. UFAHAMU

### RUNINGA NA ULIMWENGU WA LEO

Siku moja nilikuwa hotelini kisiwani Lamu, au Amu kama wanavyokiita wenyeji na rafiki yangu tukila wali na pweza. Aliingia mzee mmoja aliyefahamika kisiwani kwa ugwiji wake wa masuala ya lugha ya Kiswahili. Nilijiwa na hamu ya kumwuliza mzee huyo aliyetopea na kubobea katika Kiswahili, jinsi neno 'runinga' lilivyozuka.

"Ahh, hilo?" alishangaa kwa sauti kabla ya kuendelea, 'kijana kaa kitako nikweleze. Mswahili wa kwanza alipokiangalia kile chombo alishangaa. Kilikuwa kinaeleza na kuweka wazi mbele ya macho yake habari za ajabu . Hizi zilikuwa habari zilizotokea sehemu za mbali ambazo ni vigumu kujua zilikotokea. Ni kitu kama uvumi hivi, huku kwetu tunasema "rununu' basi ule si wa kusikia bali ni wa kuona; yaani kwa macho ambayo zamani yaliitwa maninga. Basi ikawa rununu ya mininga; mwishowe runinga' alieleza mzee huyo kwa ufasaha mkubwa.

Kila ninapokiwazia chombo kinachojulikana kama runinga au televisheni, kisa kile hufyatuka akilini na sura ya zee huyo kunijiial Tangu kuvumbuliwa kwake mwanzo mwanzo wa karne ya ishirini, runinga imekuwa mojawapo wa vyanzo vikuu vya maarifa, taarifa, elimu na burudani kwa watazamaji. Kutokana na chombo hiki tunapata picha za matendo yanayotendeka kwenye maeneo yaliyoko mbali na tuishiko. Kinatufichulia majanga yanayowafika wenzetu kutokana na mabaa ya vita au njaa; huonyesha harakati za wanasayansi za kujaribu kuvumbua mambo mapya kwenye anga zetu. Aidha runinga hutusawiria matukio ya ulimwengu na wakati huo huo yanapotokea yawe ni ya kusikitisha au ya kutuburudisha kutokana na vipindi vyake mbalimbali.

Vipindi vya runinga huwa ni ishara za elektroniki ambazo hutumwa kama mawimbi ya redio na vyombo vinavyojulikana kama setilaiti au kwa matumizi ya kebo ambazo hupitishwa ardhini. Setilaiti ina uwezo wa kubadilisha ishara hizo na kuwa sauti na picha zinazoambatana na sauti hizo.

Je, ushawahi kuwazia ni mambo yepi yanatokea katika studio za runinga hususan wakati wa kusomwa kwa taarifa ya bahari?
Aghalabu wakati wa kusomwa kwa taarifa ya habari ni sehemu ndogo sana ya studio inayoonekana. Asilimia kubwa huwa imefichwa pamoja na mashine za kila aina ambazo huhusika na uwasilishaji wa habari hizo. Aidha wahudumu wengine wanaohusika na majukumu mbalimbali kama udhibiti wa mwangaza, uelekezaji wa wanaosoma kuhusu muda uliopo, mdhibiti wa kamera zionyeshazo picha mbalimbali anayekuza picha kuhakikisha picha zimeonekana vyema. Wapo wengine wanaoshughulika na majukumu anuai ambao hawaonyeshwi.

Mbele ya msomaji wa taarifa hizo huwa kuna televisheni ndogo ambayo haionekani na ambayo humwonyesha picha zinazoonyeshwa. Aghalabu hatuwaoni wasomaji wengi wa taarifa za habari wakisoma habari zao kutoka maandishi wazi. Hali hii inatokana na kuwepo kwa kielekezi-runinga ambacho anakitumia. Msomaji huyu husoma taarifa zake kutokana na maandishi yanayoonekana kwenye *mulish* au *kiwambo* cha kielekezi hicho. Maneno hayo hukuzwa kwa njia mbili mbele ya lensi za kamera na kuweza kusomeka vizuri. Yupo opareta ambaye kazi yake kuu ni kuhakikisha kuwa

amedhibiti kasi ya maneno yanayoonekana kwenye kielekezi-runinga hicho. Pia msomaji anaweza kuongeza au kupunguza kasi ya maneno hayo kutegemea usomaji wake akitumia kifaa maalum. Hata hivyo, msomaji huwa na nakala nyingine ya habari iliyoandikwa anayoweza kuisoma iwapo pana hitilafu fulani ya kielekezi-runinga.

Wataalamu wa chumba kikuu cha kuyadhibiti matangazo hutumia vifaa maalumau vya sauti kuwakumbusha watangazaji kuhusu vipindi vya kupumzika kwa ajili ya matangazo ya biashara au mabadiliko yoyote katika mpangilio wa kipindi fulani. Huwapo pia wataalamu wanaohakikisha kuwa picha zinazopatikana kwenye runinga ni sahihi na zinakubalika. Kutokana na majukumu mbalimbali ya wanaohusika, watazamaji wanapata picha nzuri na sauti zinazoafiki picha hizo. Hii ni siri mojawapo ya siri nyingi ambazo zimefumbatwa na uvumbuzi wa kisayansi.

Kama watazamaji wa runinga labda tunaishia kukubaliana na yule mzee wa Lamu kuwa chombo hiki kina maajabu ya macho. Maajabu hayo yanatuelimisha, kutujuza, kutukumbusha na kutufanya tushirikiane na wenzetu walio mbali sana katika matukio yetu. Masafa yaliyoko kati yao yanafupishwa kwa kuwa wanatujia kwenye vyumba vyetu kama nasi tunavyofanya huko kwao.

**MASWALI**

1. Ni nini chanzo cha neno ‘runinga? (alama 2)

   **Chanzo cha runinga ni kutokana na neno rununu ya maninga kumaanisha uvumi wa kusikia na kuona kisha mwishowe ikawa runinga.**

2. Taja faida nne za runinga. (alama 2)

   **- Elimu**
   **- Burudani**

3. Tunaweza kutazama picha za runinga kutoka kwenye vituao mbalimbali vya televisheni. Ni nhia gani ipi inayotuwezesha kutazama vipindi vya runinga? (alama 2)

   **Vipindi vya runinga huwa ni ishara za elektroniki ambazo hutumiwa kama mawimbi ya redio na vyombo vinavyojulikana kama setilaiti au kwa matumizi ya kebo ambazo hupitishwa ardhini. Setilaiti ina uwezo wa kubadilisha ishara hizo na kuwa sauti na picha zinazoambatana na sauti hizo.**

4. Wakati wa kusomwa kwa taarifa za habari, kuna wataalamu mbalimbali wanaohusika. Taja watatu. (alama 3)

   **- Mdhibiti wa mwangaza**
   **- Muelekezaji wa wanaosoma kuhusu muda uliopo.**
   **- Mdhibiti wa kamera zionyeshazo picha mbalimbali.**

5. Taja mchezo mmoja wa kimataifa ulio maarufu zaidi inayotangazwa moja kwa moja kupitia runinga kote ulimwenguni. (alama 1)

   **Mpira wa kadanda.**

**B. LUGHA: (ALAMA 25)**

(a) Eleza maana ya: (alama 2)

(i) Kiimbo – **Upandaji na ushukaji wa sauti unaofanyika wakati mtu anapozungumza.**

(ii) Shadda – **Utiliaji wa mkazo kwa silabi au neno wakati wa kutamka**

(b) Onyesha matumizi mawili mawili ya alama zifuatazo: (alama 2)

**(i) Alama ya mshangao – Hutumiwa mwishoni mwa sentensi ulizi kuonyesha shaka katika sehemu fulani ya maandishi katika maswali balagha**

(ii) Mshazari – **- Kutenga nambari/tarakimu unapoandika tarehe k.m. 12/11/07 kuonyesha maneno yana maana sawa k.m. haya/voni.**
**- Katika kuandika akisani k.m. 3/5**
**- kuleta maana ya ama/au k.m. Je, nikuletee chai/soda?**

(c) Tenganisha silabi katika maneno yafuatayo kasha ubaini miundo yake.

(i) Labda (alama 2)

**Lab – da**
**k k ki**

(ii) maktaba (alama 3)

**Mak ta ba**
**kik –ki- ki**

(iii) Pambanua viambishi katika neno lifuatalo.

**Aliyempiga** **(alama 3)**

**A – Nafsi ya tatu**
**li – wakati uliopita**
**ye – kerejeshi**
**m – kitendwa**
**pig – mzizi**
**a - kiishio**

(e) Maneno haya yapo katika ngeli ipi? (alama 2)

(i) Muktadha – **U - I**

(ii) Wayo – **U – zi**

(iii) Maiti – A-Wa (kijamii) I-ZI (kisarufi)

(f) Eleza maana ya misemo ifuatayo. (alama 3)

(i) Kiinua mgongo – **malipo kama shukrani**

(ii) Enda kombo - **Potoka**

(iii) Piga milundo – **kutembea kwa miguu**

(g) Sahihisha sentensi zifuatazo:

(i) Mfereji lako ilikosa maji (alama 2)

**mfereji wake ulikosa maji**

(ii) Malengo wetu ulikuwa ya kutilia mkazo bidii shuleni.

**malengo yetu yalikuwa ya kutilia mkazo bidii shuleni**

(h) Andika sentensi hii katika hali ya udogo:

(i) Sahani zetu ni nzuri kuliko zao. (alama 2)

**Vijisahani vyetu ni vizuri kuoliko vyao**

(i) Ainisha mofimu hizi katika mofimu huru na mofimu tegemezi. (alama 3)

(i) Tunda – **Mofimu tegemezi**

(ii) Ladha – **mofimu huru**

(iii) Mwanahewa – **mofimu tegemezi**

(j) Eleza tofauti katika sentensi zifuatazo:

(i) Chakula chote kimeoza - **Hali ya ujumla, kutobakiza**

(ii) Chakula chochote kimeoza – **Kutochagua, kutobagua**

**C. FASIHI.**

(i) Taja sifa tano za vitendawili. (alama 5)

**- Huwa ni vifupi**
**- Huwa ni mtindo maalumu unaotumika kuanzia**
**- Hubuniwa kufuatia mazingira na shughuli mbalimbali za kawaida**
**- Aghalabu jibu huwa ni neno moja au maneno machacha**
**- Iwapo mteguaji atashindwa kutoa jibu, yeye hutoa 'zawadi' au mji kwa mtegaji**
**- Mtegaji anapokubali 'zawadi' au mji hutoa jibu.**

**D. ISIMU JAMII**

Taja na ueleze sifa za sajili ya mkahawani/hotelini (alama 10)

**- Msamiati maalum k.v bei, chenji, chakula, chai, soda.**
**- Mazungumzo huwa na sentensi fupi fupi**
**- Wakati mwingine mazunguzo huashiria amrishi**
**- Matumizi ya utohozxi k.m Menyu**
**- Kuchanganya ndimi k.mk mhudumu waiter.**